Ziara ya Mkuu wa Mkoa Mtwara.

Kesho Julai 10, 2017 Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mheshimiwa Halima Dendego ataanza ziara ya kikazi katika Halmashauri zote za mkoa wa Mtwara. Katika ziara hiyo itakayofanyika kwa siku Nne kila Wilaya ikianzia Wilaya ya Nanyumbu atakagua miradi mbalimbali ya Maendeleo ikiwemo Afya, Barabara, Kilimo na Maji.

Licha ya kufanya mikutano ya hadhara kwa kila Wilaya Mheshimiwa Dendego atazungumza na makundi mbalimbali katika jamii ikiwemo Wakuu wa Shule, Madiwani, Waratibu Elimu Kata, Maafisa Tarafa, viongozi wa Vyama vya Msingi na watendaji mbalimbali katika halmashauri.

Mheshimiwa Dendego amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi katika matukio mbalimbali yatakayokuwa yakifanyika katika ziara hiyo.

Imetolewa na:

Evaristy Masuha

Afisa Habari. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mtwara